# HALMASHAURI YA WILAYA YA MAGU

## MUHTASARI WA MKUTANO WA KAWAIDA WA BARAZA LA MADIWANI KWA AJILI YA KUPITIA TAARIFA ZA UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO KWA KIPINDI CHA ROBO YA TATU JANUARI - MACHI 2023/2024 ULIOFANYIKA TAREHE 8-9/05/2024 KATIKA UKUMBI WA CCM-MAGU

**WAJUMBE WALIOHUDHURIA: -**

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1. | Mhe. Mpandalume S. Mpandalume | Diwani Kata ya Nyigogo | Mwenyekiti |
| 2. | Mhe. Marco J. Kabadi | Diwani kata ya Kisesa | M/Mwenyekiti |
| 3. | Mhe. Edda Benjamin | Diwani V/Maalum kata ya Kandawe | Mjumbe |
| 4. | Mhe. Gunze Philipo | Diwani kata ya Mwamanga | Mjumbe |
| 5. | Mhe. Nduhi L. Kabadi | Diwani kata ya Mwamabanza | Mjumbe |
| 6. | Mhe. Secilia E. Hima | Diwani V/maalum kata ya Kabila | Mjumbe |
| 7. | Mhe. Gilang’hinda Busiga | Diwani kata ya Nkungulu | Mjumbe |
| 8. | Mhe. Rebeca J. Kipeja | Diwani V/Maalum Kata ya Kahangara | Mjumbe |
| 9. | Mhe. Ng’wanabuta Enos | Diwani kata ya Lutale | Mjumbe |
| 10. | Mhe. Gerald Paul | Diwani Kata ya Ng’haya | Mjumbe |
| 11. | Mhe. Peter Deogratius | Diwani kata ya Jinjimili | Mjumbe |
| 12. | Mhe. John N. Ngagaja | Diwani Kata ya Shishani | Mjumbe |
| 13. | Mhe. Faustine Makingi | Diwani kata ya Sukuma | Mjumbe |
| 14. | Mhe. Velina E. Makwandi | Diwani kata ya Isandula | Mjumbe |
| 15. | Mhe. Mary Kaligi | Diwani V/Maalum kata ya Kitongosima | Mjumbe |
| 16. | Mhe. Hilder A. Mdachi | Diwani V/maalum kata ya Kisesa | Mjumbe |
| 17. | Mhe. Stella Maya | Diwani V/maalum kata ya Isandula | Mjumbe |
| 18. | Mhe. Petro L. Matonange | Diwani kata ya Buhumbi | Mjumbe |
| 19. | Mhe. Lucas M. Zabron | Diwani kata ya Lubugu | Mjumbe |
| 20. | Mhe. Marco Minzi | Diwani Kata ya Bukandwe | Mjumbe |
| 21. | Mhe. Bunyanya K. John | Diwani kata ya Bujora | Mjumbe |
| 22. | Mhe. Kiswaga B. Destery | Mbunge Jimbo la Magu | Mjumbe |
| 23. | Mhe. Deleli L. Mazoya | Diwani kata ya Bujashi | Mjumbe |
| 24. | Mhe. Machibula L. Deus | Diwani kata ya Kahangara | Mjumbe |
| 25. | Mhe. Silas C. Kipeja | Diwani Kata ya Kitongosima | Mjumbe |
| 26. | Mhe. Mashaka Mathias | Diwani kata ya Magu Mjini | Mjumbe |
| 27. | Mhe. Herbert G. Faustine | Diwani kata ya Kongolo | Mjumbe |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 28. | Mhe. Hilali Elisha | Diwani kata ya Nyanguge | Mjumbe |
| 29. | Mhe. Butogwa B. Mayala | Diwani V/Maalum kata ya Bujora | Mjumbe |
| 30. | Mhe. John M. Mitubo | Diwani kata ya Chabula | Mjumbe |
| 31. | Mhe. Sambo M. Lupondije | Diwani kata ya Itumbili | Mjumbe |
| 32. | Mhe. Anna P. Makula | Diwani kata ya Shishani | Mjumbe |
| 33. | Mhe. Edward Kihamba | Diwani Kata ya Kabila | Mjumbe |
| 34. | Mhe. Lucas Bomoa | Diwani Kata ya Kandawe | Mjumbe |
| 35. | Mhe. Diana Philemoni | Diwani V/maalum Kata ya Kitongosima | Mjumbe |

**WAJUMBE WASIOHUDHURIA KWA TAARIFA:**

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Mhe. Dr. Stergomena Tax | Mbunge Mteule |
| 2. | Mhe. Mary F. Masanja | Mbunge Viti Maalum |

**WATENDAJI WALIOHUDHURIA:**

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Bw. Mohamed Kyande | Kaimu Mkurugenzi Mtendaji H/W ya Magu |
| 2. | Bw. Henry J. Sadatale | Mkuu wa Idara ya Utawala na Usimamizi wa Rasilimali watu |
| 3. | Bw. Peter M. Mujaya | Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Michezo, Utamaduni na Sanaa |
| 4. | Machibya N. Lutema | Mkuu wa Idara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi |
| 5. | Bw. Paschal Mashamba | Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini. |
| 6. | Bw. Mwagala Masunga | Bw. Mwagala Masunga |
| 7. | Bi. Leticia Nyakahinga | Kaimu Mkaguzi Mkuu na Mdhibiti Ubora wa Shule |
| 8. | Bw. Ngussa M. Buyamba | Mkuu wa Kitengo cha Maliasili na Uhifadhi wa Mazingira |
| 9. | Adv. John Ngalula | Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Sheria |
| 10. | Bw. Peter M. Manoko | Mkuu wa Kitengo cha Usimamizi wa Ununuzi |
| 11. | Bw. Pastory Mkaruka | Mkuu wa Idara ya Mipango na Uratibu |
| 12. | Bw. Yusuph Digossi | Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini. |
| 13. | Bi. Juliana L. Nyambalya | Kaimu Mkuu wa Idara ya Miundombinu Maendeleo ya Vijiji na Mijini |
| 14. | Bw. Amandus L. Mboya | Mkuu wa Idara ya Maendeleo ya Jamii |
| 15. | Bw. Alphonce Awaki | Mkuu wa Sehemu ya Kilimo |
| 16. | Bi. Emmanuela P. Chacha | Kaimu Katibu TSC |
| 17. | Bw. Francisco M. Ndazi | Kaimu Mkuu wa Kitengo cha usimamizi wa taka na usafi wa mazingira |

| | |
|---|---|
| 18. Bw. Joseph J. Mtengu | Mkuu wa Kitengo cha Fedha na Uhasibu |
| 19. Bi. Kuruletela Florence | Mkuu wa kitengo cha Ukaguzi wa ndani. |
| 20. Bi. Glory V. Mtui | Mkuu wa Divisheni ya Elimu ya Awali na Msingi |
| 21. Bi. Beatrice B. Balige | Mkuu wa Divisheni ya Elimu Sekondari |
| 22. Bw. Wilfred Majigo | Mkuu wa Divisheni ya Ardhi |
| 23. Bw. Eusebius Chanjali | Kaimu Mkuu wa Divisheni ya Huduma za Afya, Ustawi wa Jamii na Lishe |
| 24. Bw. Simioni Mwita | Kaimu Afisa Usafirishaji. |
| 25. Bi. Martha Godi | Afisa Utumishi |
| 26. Bw. Fundikira Saidi | Mtendaji Mkuu wa Mamlaka ya Mji Mdogo wa Magu. |
| 27. Dr. Daniel Sanyenge | Mratibu TASAF |
| 28. Bw. Festus P. Kisanga | Kaimu Mkuu wa Idara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji |

**KAMATI YA ULINZI NA USALAMA:**

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Bi. Anna H. Mbao | Kaimu Mkuu wa Wilaya |
| 2. | A/Insp Victor Adam | Afisa Usalama |
| 3. | Bw. Elias D. Mwandobo | Mkuu wa Usalama (W) |
| 4. | Sp. Kiyelu Y. Bayinga | Mkuu wa Magereza (W) |
| 5. | Bw. Francis Nyerere | Kaimu Kamanda wa TAKUKURU (W) |
| 7. | A/Insp Gastone C. Tigulabwa | Kamanda wa Zimamoto (W) |
| 8. | Sp. Haji F. Makame | Mkuu wa Polisi (W) |

**WAGENI WAALIKWA:**

| | |
|---|---|
| 1. Bw. Japhet Barton | Kaimu Meneja MWAUWASA (W) |
| 2. Bw. Lubapula Mayombya | Kaimu Meneja MWAUWASA (W) |
| 3. Bw. Emmanuel kalagara | Meneja wa TANROAD |
| 4. Bw. Musa Z. Mzimbiri | Meneja TARURA (W) |
| 5. Bw. Enos N. Kalambo | Mwenyekiti CCM (W) |

**MAAFISA TARAFA**

| | |
|---|---|
| 1. Bw. Emmanuel M. Ndillah | Afisa Tarafa Itumbili |
| 2. Bw. Anthony M. Ntarle | Afisa Tarafa Sanjo |
| 3. Bi. Grace M. Msilanga | Afisa Tarafa Ndagalu |
| 4. Bi. Silyvia L. Mayala | Afisa Tarafa Kahangara |

## WATENDAJI WA KATA

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Bw. Evodius Mushema | Mtendaji wa Kata ya Mwamabanza |
| 2. | Bi. Salome Julius | Mtendaji Kata ya Bujora |
| 3. | Bw. Ernest M. Mkama | Mtendaji wa Kata ya Lubugu |
| 4. | Bw. Azimio Gervas | Mtendaji wa Kata ya Kahangara |
| 5. | Bw. Ezekiel W. Segeredi | Mtendaji wa kata ya Kitongosima |
| 6. | Bw. Essau Gwangimeza | Mtendaji wa Kata ya Jinjimili |
| 7. | Bw. Emmanuel C. Saendah | Mtendaji wa Kata ya Mwamanga |
| 8. | Bw. Wilbroad K. Mbuga | Mtendaji wa kata ya Nyanguge |
| 9. | Bi. Eunice S. Sangila | Kaimu Mtendaji wa Kata ya Kongolo |
| 10. | Bw. John C. Mabiti | Mtendaji wa Kata ya Isandula |
| 11. | Bw. Daniel J. Sahani | Mtendaji kata ya Chabula |
| 12. | Bw. Ismail V. Oyuga | Mtendaji wa Kata ya Kisesa |
| 13. | Bw. Philipo J. Lusesa | Mtendaji wa Kata ya Nyigogo |
| 14. | Bw. Michael Brasio | Mtendaji wa kata ya Buhumbi |
| 15. | Bi. Catherine C. Matutu | Mtendaji wa Kata ya Shishani |
| 16. | Bw. Jeremiah A. Kalwani | Mtendaji wa Kata ya Ng'haya |
| 17. | Bw. Juma R. Kashilimu | Mtendaji wa Kata ya Magu Mjini |
| 18. | Bw. Leonard L. Nzabhayanga | Mtendaji wa Kata ya Kabila |
| 19. | Bi. Devotha M. Robert | Mtendaji wa Kata ya Sukuma |
| 20. | Bi. Lina D. Amata | Mtendaji kata ya Itumbili |
| 21. | Bw. Emmanuel C. Sengerema | Mtendaji wa Kata ya Bukandwe |
| 22. | Bw. Ichobe M. Nyasanga | Mtendaji wa kata ya Bujashi |
| 23. | Bw. Charles M. Mabona | Mtendaji wa Kata ya Nkungulu |
| 24. | Bw. Victor M. Kisamu | Mtendaji wa Kata ya Lutale |
| 25. | Bw. Patrick Mkame | Mtendaji Kata ya Kandawe |

## SEKRETARIETI:

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Bi. Happiness J. Mbalilaki | Mwandishi wa Vikao |
| 2. | Bi. Judith J. Aron | Mwandishi wa Vikao |
| 3. | Bw. Jordan F. Mchongi | Mwandishi wa Vikao |

**MUHT. NA. 23/2023/2024: - KUFUNGUA MKUTANO:**

Katibu alimkaribisha Mwenyekiti ili afungue mkutano wa Baraza la Madiwani kwa ajili ya kupitia taarifa za utekelezaji robo ya tatu Januari – Machi, 2023/2024.

Mwenyekiti aliwakaribisha wajumbe na wageni waalikwa kwenye mkutano wa kawaida kwa ajili ya kupitia taarifa mbalimbali za utekelezaji pamoja na taarifa kutoka katani. Alifungua kikao mnamo saa 4.00 asubuhi.

**MUHT. NA 24/2023/2024: - KURIDHIA AGENDA:**

Mwenyekiti aliwaongoza wajumbe kupitia agenda zilizoandaliwa kwa ajili ya mkutano kama ifuatavyo: -

1. Kufungua mkutano
2. Kuridhia agenda
3. Taarifa za utekelezaji kutoka katani
4. Maswali ya papo kwa papo
5. Kusoma na kuthibitisha Muhtasari wa mkutano wa Baraza la madiwani uliofanyika tarehe 16-17/02/2024
6. Kuwasilisha taarifa za kamati za kudumu za Halmashauri kwa kipindi cha Januari - Machi, 2024.
    - Kamati ya Elimu, Afya na Maji
    - Kamati ya Uchumi, Ujenzi na Mazingira
    - Kamati ya UKIMWI (CMAC)
    - Kamati ya Fedha, Uongozi na Mipango
7. Taarifa ya utekelezaji miradi ya maendeleo katika kipindi cha robo ya tatu Januari - Machi, 2024
8. Maswali kutoka vyama vya siasa
9. Mapendekezo ya kugawa jimbo la Magu
10. Taarifa za Kiutumishi
11. Matangazo kutoka kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya
12. Mengineyo
13. Kufunga mkutano

**MUHT. NA. 25/2023/2024: TAARIFA ZA UTEKELEZAJI KUTOKA KATANI**

Kata zilizowasilisha taarifa za utekelezaji kutoka kata ni kama ifuatavyo; -

Kata ya Bujora, Lubugu, Nyigogo, Lutale, Ng’haya, Mwamabanza, Kitongosima, Jinjimili, Kisesa, Shishani, Itumbili, Kahangara, Nkungulu, Magu mjini, Chabula, Sukuma**,** Mwamanga, Buhumbi, Isandula, Nyanguge, Bujashi, Bukandwe, Kongolo, Kabila, Lutale

**MUHT. NA. 26/2023/2024: MASWALI YA PAPO KWA PAPO**

Hakuna maswali ya papo kwa papo yaliyowasilishwa mezani kwa Mwenyekiti.

**MUHT. NA. 27/2023/2024: KUSOMA NA KUTHIBITISHA MUHTASARI WA MKUTANO WA BARAZA LA MADIWANI ULIOFANYIKA TAREHE 16 - 17/02/2024**

Mwenyekiti aliwaongoza wajumbe kupitia muhtasari ukurasa kwa ukurasa ili kujiridhisha kuwa kilichoandikwa ndicho kilichojadiliwa kisha kuupitisha kuwa kumbukumbu halali za Halmashauri.

**MUHT. NA. 28/2023/2024: KUWASILISHA TAARIFA ZA KAMATI ZA KUDUMU ZA HALMASHAURI KWA KIPINDI CHA JANUARI HADI MACHI, 2023/2024**

Wenyeviti wa kamati za kudumu za Halmashauri waliwasilisha taarifa za kamati katika kipindi cha robo ya tatu Januari hadi Machi, 2023/2024 ili zijadiliwe na wajumbe kama ifuatavyo: -

- Kamati ya UKIMWI
- Kamati ya Elimu, Afya na Maji
- Kamati ya Uchumi, Ujenzi na Mazingira
- Kamati ya Fedha, Uongozi na Mipango

Baada ya kuwasilishwa kwa taarifa wajumbe walizipokea na kuwa kumbukumbu za Halmashauri.

**MUHT. NA. 29/2023/2024: TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO KWA KIPINDI CHA ROBO YA TATU JANUARI HADI MACHI, 2024**

Mkuu wa Idara ya utawala na Usimamizi wa Rasilimali watu kwa niaba ya Mkurugenzi Mtendaji aliwasilisha taarifa ya utekelezaji katika kipindi cha robo ya tatu Januari hadi Machi, 2024. Wajumbe walipokea taarifa hiyo na hapakuwepo na mjadala hivyo walipitisha kuwa kumbukumbu ya Halmashauri ya Wilaya.

**MUHT. NA. 30/2023/2024: MASWALI KUTOKA VYAMA VYA SIASA**

**Swali na.01:**

Lini miradi ya maji Mahaha, Iseni na Buhumbi itakamilika?

**Majibu:**

Mradi wa maji Mahaha utakamilika Julai, 2024 mradi huu umechelewa kuanza kwa sababu ya hatua za manunuzi ambazo kwa sasa zimekamilika na fedha zimekwishapokelewa.

Mradi wa Nyang'hanga – Iseni unategemea kukamilika tarehe 30/06/2024, mradi huu ukikamilika vijiji vya Iseni, Nyang'hanga, Buhumbi, Nyashoshi na Mwamibanga watapata huduma ya maji. Mradi huu una sehemu kuu mbili ambapo ni ujenzi wa miundombinu na ununuzi wa pampu, mzabuni wa pampu anaendelea na ununuzi huo.

**Swali na. 02:**

Lini Vitongoji vya Kashishi na Inolelo vitawekewa umeme.

**Majibu:**
Mpango wa usambazaji umeme Wilaya ya Magu umeendelea kutekelezwa kupitia mpango wa REA awamu ya tatu mzunguko wa pili. Hivyo kumalizika kwa awamu hii umeifanya Wilaya ya Magu kufikiwa na umeme kwenye Vijiji 82, awamu inayofuata ni kusambaza umeme kwenye Kijiji/Vijiji husika kwa kupitia Vitongoji vyote. Kwa sasa Wilaya ya Magu ina Vitongoji 508 na kati ya hivyo Vitongoji 202 pekee ndiyo vimefikiwa na umeme na Vitongoji 306 bado havijafikiwa na umeme kwa awamu zilizopita. Serikali kupitia REA itaanza mpango wa utekelezaji wa kupeleka umeme kwenye Vitongoji hivyo kuanzia mwanzoni mwa mwaka wa fedha 2024/2025 mwezi wa 7. Hivyo tuendelee kuvuta subira wakati utekelezaji unakwenda kuanza.

Mheshimiwa Diwani Kata ya Bujashi alisema kuwa mahitaji ya umeme bado ni makubwa hivyo TANESCO wajitahidi kuboresha huduma, Vitongoji vingi havijapata umeme, hivyo wajitahidi kutekeleza ili wananchi wapate huduma ya umeme.

Mheshimiwa Diwani Kata ya Mwamanga aliuliza ni lini Vijiji vya Kashishi na Inolelo vitapatiwa umeme. Alishauri Vitongoji vyenye taasisi kama shule vipatiwe vipaumbele katika huduma ya usambazaji wa umeme.

Meneja wa TANESCO alisema kuwa mchakato wa uwekaji umeme unaendelea, suala la Vijiji vya Kashishi na Inolelo linatekelezwa na REA.

Mheshimiwa Diwani Kata ya Shishani alisema kuwa shule tatu katika Kata yake hazina umeme, hivyo aliomba wapatiwe huduma hiyo.

Meneja wa TANESCO alisema kuwa shule hizo bado hazijafanyiwa makadirio ya gharama hivyo timu ya wataalam kutoka TANESCO wataenda ili kufanya makadirio ya gharama ili kufikisha huduma ya umeme.

Mheshimiwa Diwani Kata ya Kahangara alisema kuwa uwepo wa umeme unasaidia kufungua ajira hivyo alishauri TANESCO wajitahidi kusambaza huduma ya umeme ili wananchi waweze kupata na kubuni mbinu za kufungua huduma zinazotokana na umeme katika maeneo mbalimbali.

**Swali na.03:**

Daraja/Kalvati shule ya msingi Moha ni lini litatengenezwa ikiwa ni pamoja na daraja la Mwatelesha na Bugatu.

**Majibu:**

Daraja/kalvati katika shule ya msingi Moha na daraja katika barabara ya Mwatelesha imeombewa fedha kwenye bajeti ya dharura Makao Makuu kwa hiyo bajeti itakapokuja utekelezaji utaanza. Utekelezaji wa ujenzi daraja katika barabara ya Bugatu litawekwa kwenye bajeti ya mwaka 2024/2025.

Mheshimiwa Diwani kata ya Ng'haya alisema kuwa mvua zimeharibu daraja hilo ilihali linategemewa sana kwa shughuli za kila siku za wananchi. Aliomba kuhakikishiwa na Meneja wa TARURA kama kuna uhakika wa kutengeneza daraja hilo mwaka wa fedha 2024/2025.

Meneja wa TARURA alisema kuwa changamoto ya mvua imeathiri barabara nyingi kuna fedha za dharura zimepokelewa kwa ajili ya kukarabati baadhi ya barabara, hivyo aliwatoa wasiwasi wajumbe kuwa kalvati hiyo itajengwa.

Mkuu wa Idara ya Mipango na Uratibu alisema kuwa kuna andiko lilioandikwa na Idara ya Mipango kwa kushirikiana na ofisi ya TARURA kwenda TAMISEMI kwa ajili ya kuomba fedha za dharura zitakazotumika kutengeneza barabara zilizoathiriwa na mvua.

Mheshimiwa Diwani kata ya Bujora alishauri wataalam wanapokwenda kwenye maeneo ya matengenezo wawashirikishe wananchi wa eneo hilo kwa kuwa wanaweza kuwashauri na maelekezo ya kuwasaidia wataalam katika kazi zao.

Mheshimiwa Diwani kata ya Kahangara alimshukuru Meneja wa TARURA kwa utendaji kazi wake kwa kuwa wajumbe wengi wa Baraza wanamuamini katika utendaji kazi. Alimuuliza ni lini daraja la mto Nyang'oma litajengwa.

Mwenyekiti wa kikao alimuelekeza Meneja wa TARURA afanyie kazi suala la daraja la mto Nyang'oma.

**MUHT. NA. 31/2023/2024: MAPENDEKEZO YA KUGAWA JIMBO LA MAGU**

Mkuu wa Idara ya Utawala na Usimamizi wa Rasilimali watu kwa niaba ya Mkurugenzi Mtendaji aliwasilisha mapendekezo ya kugawa Jimbo a Magu. Wajumbe waliipokea taarifa hiyo na kisha kujadili kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Diwani Kata ya Isandula alikubaliana na pendekezo la kugawa Jimbo la Magu na kusema kuwa Jimbo ni kubwa sana lina vitongoji 200 ambapo ni kazi kubwa kuvifikia. Alisema kugawa Jimbo itasaidia kupata fedha mara mbili kutoka kwa wabunge wa majimbo hayo na hivyo maendeleo yataonekana kiurahisi.

Mheshimiwa Diwani Kata ya Bujora aliunga mkono pendekezo la kugawa jimbo la Magu alishauri vikao vya juu kama vikao vya Mkoa na DCC wabariki pendekezo hilo.

Mheshimiwa Diwani Kata ya Bukandwe aliunga mkono pendekezo la kugawa Jimbo la Magu na kusema kuwa sababu zilizotolewa zinajitosheleza. Alisema kuwa Wilaya ya Magu ina kata kubwa ambazo pia zinastahili kukatwa na kuwa majimbo alizitaja kata hizo kuwa ni BUJASHI, KAHANGARA, NG'HAYA, KANDAWE, BUKANDWE, MWAMANGA na SHISHANI kutokana

na ukubwa na wingi wa watu katika Kata hizo, alishauri zifanyiwe mchakato wa kuzigawa kuwa majimbo. Aliongelea Kitongoji cha Mwahole kutokana na ramani ukubwa na wingi wa watu pia kitongoji hicho kinastahili kuwa jimbo. Dhamira ya kugawa maeneo makubwa na yenye wingi wa watu ni kusogezana kuboresha huduma hivyo alishauri dhamira hiyo izingatiwe ili huduma bora iwafikie wananchi.

Mwenyekiti wa kikao aliwauliza wajumbe ni wangapi walikubaliana na wazo la kuligawa jimbo, wajumbe wote walikubali kwa kunyoosha mikono kisha Baraza la Madiwani kupitia mkutano wake waliridhia na kushauri kuwepo kwa majimbo mawili ambayo ni Jimbo la Sanjo na Jimbo la Magu. Waliridhia Jimbo la Sanjo litaundwa na tarafa mbili ambazo ni Kahangara na Sanjo na Jimbo la Magu litaundwa na tarafa mbili ambazo ni Itumbili na Ndagalu.

**MUHT. NA. 32/2023/2024: TAARIFA ZA KIUTUMISHI**

Baada ya baraza la madiwani kujigeuza na kuwa kama kamati taarifa za kiutumishi ziliwasilishwa na kujadiliwa.

**SALAMU KUTOKA MEZA KUU NA MUALIKWA KUTOKA NIDA WILAYA YA MAGU**

Mwenyekiti aliwakaribisha wajumbe wa meza kuu na mgeni kwa ajili ya kuongea na wajumbe wa kamati.

Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi (CCM) aliwapongeza kwa kikao kizuri na michango mizuri waliyotoa kwenye mkutano. Alisisitiza juu ya fedha za miradi zinapoletwa na wafadhili ufuatiliaji ufanyike thamani ya fedha kwenye miradi husika ijulikane. Alisema kuwa tunaelekea kwenye kipindi cha uchaguzi wa Serikali za mtaa, hivyo ni vyema tushirikiane tushikamane, tuombee zoezi la uchaguzi na kuendelea kukisemea vizuri chama cha mapinduzi.

Kaimu Mkuu wa Wilaya aliwapongeza watendaji, madiwani na watumishi kwa kazi nzuri wanazofanya. Alisisitiza maoni na changamoto zote zilizotolewa kutoka kwa wajumbe zifanyiwe kazi. Aliongelea umakini uchukuliwe dhidi ya mvua zinazonyesha na wananchi waelimishwe hususani watoto wasichezee kwenye madimbwi yenye maji. Vyanzo vya mapato viboreshwe inapotokea vimepata changamoto au kuharibika. Alimalizia kwa kusema kuwa tarehe 30/05/2024 mpango uliopo ni watumishi wa Halmashauri kuhamia kwenye jengo lao la Ilungu, hivyo mheshimiwa Mkuu wa Wilaya amekuwa akifuatilia kwa ukaribu juu ya hatua ya ukamilishaji iliyofikiwa.

Makamu mwenyekiti alianza kwa kuwapongeza watumishi waliopata zawadi za utumishi bora siku ya meimosi. Alisisitiza Wakuu wa Idara ya Sekondari na Idara ya Elimu ya Awali na Msingi wafuatilie suala la upatikanaji wa huduma ya chakula cha mchana kwa wanafunzi kwakuwa ni muhimu sana.

Aliongelea suala la mapato na kusisitiza yaendelee kufuatiliwa na kukusanywa, alimalizia kwa kuunga mkono pendekezo la kugawa Jimbo la Magu na kusema kuwa ni jambo zuri ambalo lina manufaa na litasaidia katika kuleta maendeleo kwa wananchi.

**MUHT. NA. 33/2023/2024: MATANGAZO KUTOKA KWA MKURUGENZI MTENDAJI WA HALMASHAURI YA WILAYA**

Kaimu Mkurugenzi aliwapongeza wajumbe kwa namna kikao kilivyoendeshwa vizuri. Alizungumzia suala la ugawaji wa vyandarua ambapo ni zoezi la wataalam kutoka TAMISEMI,

Wizara ya Afya na shirika la PMY hivyo elimu itolewe ili wananchi wawe tayari kutoa ushirikiano na kugawiwa vyandarua hivyo na wavitumie kwa matumizi kama yalivyoelekezwa.

Alizungumzia sheria ndogo kuwa zimeanza kutumika, Watendaji wa Kata na Vijiji tayari wamepewa sheria hizo. Alisisitiza elimu izidi kutolewa katika vikao vya maendeleo ya kata (WDC) na vikao vya kisheria ili kuhakikisha wananchi wanapata uelewe na kuongozwa na sheria hizo katika shughuli zao za kila siku.

**MUHT. NA. 34/2023/2024: MENGINEYO**

Hapakuwepo na mengineyo